

WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA SIKU 10 KUANZIA TAREHE 15 HADI 25 SEPTEMBER, 2026



Imeandaliwa na;

Bodi ya Maji Bonde la
Wami/Ruvu

P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania

Phone: 0800114031 / 0800114032

E-mail barua@wrbwb.go.tz

Website: www.wrbwb.go.tz


Septemba, 2026

1. UTANGULIZI

Yaliyomo

1. UTANGULIZI
2. UTABIRI WA HALI YA MAJI
3. ATHARI
4. USHAURI
5. HITIMISHO

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kuzingatia vituo vilivopo katika *Catchment* (**Kielelezo Na.1**) kwa kipindi cha kuanzia tarehe 15 Septemba hadi 25 Septemba, 2026. Utabiri huu unalenga kuwezesha wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kufahamu mwenendo wa wingi wa maji katika mto huo ili waweze kujua hali ya mwenendo wa wingi wa maji. Aidha, utabiri huu umezingatia utabiri wa hali ya mvua na Joto zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania



(TMA).

Kielelezo Na.1: Vituo vilivyotumika kufanya utabiri wa wingi wa Maji katika *Catchment* ya Mto Ruvu

2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu umefanyika kwa siku kumi zijazo kuanzia tarehe 15 Septemba hadi 25 Septemba, 2026 kama inavyoonekana katika Jendwali Na. 1; -

Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu.

Jina la Mto	Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji	Kielelezo
Ruvu	Utabiri unaonesha kuwa wingi wa maji utaendelea kupanda hadi juu ya wastani ukilingaisha na wastani wa muda mrefu (2009–2024). Aidha, kuongezeka kwa kiwango cha maji inatokana na Mvua zilizonyesha katika safu za Milima ya Uluguru ambayo ndiyo chanzo cha Mto Ruvu. Pia, kiwango cha maji kilichopo kwa sasa ambayo ni lita 12,120 kwa sekunde pamoja na matarajio ya siku kumi zijazo ni himilivu na kinatosheleza mahitaji ya sekta mbalimbali, ikiwemo mahitaji ya maji ya majumbani yanayohudumiwa na mitambo ya DAWASA ya Ruvu Juu na Ruvu Chini. Kwa sasa, mahitaji ya maji ni lita 6,000 kwa sekunde. (Kielelezo).	

3. USHAURI KWA SEKTA MBALIMBALI

Bodi inapenda kuwashauri watumiaji wa Maji katika sekta ya Kilimo, Ujenzi, Madini, Utalii, Mifugo na uvuvi, Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuendelea kutumia kiasi cha maji kilichopo kwa ufanisi.

4. HITIMISHO

Bodi itaendelea kutoa taarifa ya mwenendo wa wingi wa maji kila baada ya siku kumi na kuwahabarisha watumiaji na Mto Ruvu ili waendelea kuchukua hatai za tahadhari dhidi ya kuongezeka/kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa siku zijazo.